


## **FAHAMU ZAIDI KUHUSU VIRUSI VYA CORONA (COVID-19)**

Virusi vya corona (coronavirus) ni kundi la virusi vinavyoweza kusababisha magonjwa kwa wanyama (mamalia na ndege) lakini pia kwa binadamu. Inaaminiwa ni virusi vilivyohama kutoka kwa wanyama na kuathiri binadamu pia.



**Virusi vya corona viro katika makundi makubwa manne, yakiwemo SARS, MERS, COVID-19 na NCOV.**

### **1. SARS – Severe Acute Respiratory Syndrome.**

Ni homa ya mafua makali inayosababisha /tokana na virusi vya corona. SARS iligundulika mnamo November mwaka 2002, kusini ya China, kesi zaidi ya 8000 ziliripotiwa na watu 774 waliripotiwa kufariki dunia kutohana na SARS. Kati ya November 2003 na Julai 2003, SARS iliripotiwa kufika katika nchi 17 duniani. Tangu mwaka 2004 hakuna mgonjwa mwingine wa SARS aliyeripotiwa. Hata Hivyo ,mwaka 2017 wanasyansi waligundua virusi vya corona vyenye kusababisha SARS kwenye popo, jimbo la Yunnan, China.

## **2. MERS—Middle East Respiratory Syndrome.**

MERS ni maarufu kama homa ya ngamia (camel), ukiita homa ya mafua ya mashariki ya kati sio vibaya pia. MERS ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona. Uligundulika kwa mara ya kwanza Saudi Arabia mwaka 2012 na mpaka mwaka 2017, kesi takriban 2000 zilishari potiwa. Asilimia 36 ya watu walioripotiwa kupata maambukizi walifariki dunia.

## **3. COVID-19 –Corona Virus Disease 2019.**

Hili ndo toleo jipya la virusi vya corona linaloitikisa dunia kwa sasa. Ni mwendelezo uleule wa mashambulizi makali ya virusi vya corona. COVID-19 Kama ilivyo kwa virusi vingine vyote vya corona, asili yake ni maambukizi kutoka kwa wanyama (popo) kwenda kwa binadamu.

## **4. NCOV- Novel Corona Viruses**

Kwa mujibu wa ripoti ya shirika la afya ulimwenguni (WHO) Januari 21, mwaka 2020, mgonjwa wa kwanza mwenye NCOV aligundulika Jamhuri ya Korea (Korea Kusini). Aliyegundulika ni mwanamke raia wa china mwenye umri wa miaka 35, mkazi wa Wuhan, Hubei China.

Kwa kifupi kabisa, virusi vya corona viro kwenye kundi la Zoonotic, asili yake wanyama. Zoonotic au Zoonosis ni maambukizi ya kibakteria, virusi na parasaiti, kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

## **NJIA ZA KUSAMBA KWA VIRUSI VYA CORONA**

Njia za kusambaa kwa virusi vya corona kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa binadamu mwingine: -

1. Njia ya hewa (Kukohoa au kupiga chafya). Mtu mwenye corona akikohoa jirani na asiyekuwa na virusi hivyo, kasha asiyekuwa navyo akivuta hewa ndani, uwezekano wa kupata maambukizi ni mkubwa. Njia hiyo inaitwa respiratory droplets.
2. Njia nyingine ambayo inaelezwa na wataalamu mbalimbali duniani ni kugusana au kukaribiana kwa angalau futi sita na mwathirika wa virusi vya corona. Uwezekano wa kupata maambukizi ni zaidi ya asilimia 50. Njia nyingine ni kupeana mikono.

## **CORONA INAVYOENEA**

Mpaka machi 12 2020 watu Zaidi 125000 walikuwa wameshaambukizwa COVID-19 katika nchi 80 duniani.Kati ya hao,watu 4800 walishafariki dunia.Watu 68000 wameripotiwa kupona COVID-19 Duniani kote.Takwimu hizo ni kwa mujibu wa kituo cha sayansi cha chuo kikuu cha John Hopkins,kilichopo Baltimore, Maryland, Marekani.

Mpaka sasa hakuna kinga wala tiba ya COVID-19. Kwa mujibu wa madaktari wa china ambako maambukizi ni makubwa na vifo ni vingi,kupona kwa mgonjwa mwenye COVID-19 hutegemea uimara wa kinga za mwili za mwathirika.

Kwamba idadi kubwa ya watu wanaopona COVID-19 wanabebwa na uimara wa kinga zao kuliko matibabu wanayopatiwa. Na hilo ni angalizo kuwa kwa mtu ambaye kinga za mwili wake zina shaka au zimeshuka au anaumwa na maradhi mengine, anapoambukizwa COVID-19 uwezekano wa kupona unapungua.

## **DALILI ZA MGONJWA WA CORONA**

### **1. Dalili zinazoonekana mara kwa mara.**

- a) Homa
- b) Kikohozi kikavu baada ya siku 2-7
- c) Uhemaji wa tabu
- d) Maumivu ya mwili
- e) Kuharisha
- f) Kukosa hamu ya kula

### **2. Dalili za mara chache**

- a) Homa ya mapafu
- b) Homa kali
- c) Kukohoa damu
- d) Figo kushindwa kufanya kazi

## **NJIA ZA KUPUNGUZA MAAMBUKIZI.**

- 1) Epuka maeneo ya mikusanyiko
- 2) Usipeane mikono, pia epuka kugusa macho,pua na kinywa.

- 3) Nawa mikono kwa sabuni (medicated) na maji tiririka walau kwa sekunde 20
- 4) Jifunike kwa tishu au kitambaa ,unapokohoa au kupiga chafya,kisha tupa tishu uliyotumia kwenye chombo cha taka au tunza kitambaa chako vizuri.
- 5) Usishirikiane vitu na muathirika pia epuka kukaribia karibu na muathirika wa COVID-19.
- 6) Safisha kwa dawa ya kuuwa vimelea kwenye vitu vinavyoguswa mara kwa mara

Tumuombe Mungu maambukizi yasiendelee kwa kasi iliyopo. Athari kubwa za ugonjwa ni kiafya na kiuchumi. Ugonjwa huu ni hatari na unatishia maendeleo ya mwanadamu. Tuombe udhibiti kwa wagonjwa wenyewe COVID-19, wapone bila kuambukiza wengine.

**IMEANDALIWA NA:** Adam F. Zuberi